HOTUBA YA MTENDAJI MKUU WA WAKALA YA SERIKALI MTANDAO, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA DK. JABIRI KUWE BAKARI KWENYE SHEREHE YA UZINDUZI RASMI WA WAKALA MPYA ZA SERIKALI, UKUMBI WA KARIMJEE TAREHE 11 JULAI 2012

Mh. Katibu Mkuu Kiongozi,

Ndugu Makatibu Wakuu wa Wizara Mliopo;

Ndugu Naibu Makatibu Wakuu Mliopo;

Ndugu Wenyeviti na Wajumbe mbalimbali wa Bodi za Ushauri;

Ndugu Watendaji Wakuu wa Wakala za Serikali;

Ndugu Wakurugenzi Mbalimbali;

Watendaji Mbalimbali wa Serikali;

Ndugu Wageni Waalikwa;

Ndugu Wanahabari

Mabibi na Mabwana.

Habari za Jioni,

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kwa niaba ya watumishi wa Wakala ya Serikali Mtandao na mimi binafsi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana katika tukio hili muhimu kwetu sisi kama Wakala, lakini pia kwa Taifa zima. Aidha, nichukue nafasi hii kuungana na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi Umma, Makatibu Wakuu wengine na Watendaji Wakuu wenzangu katika kukushukuru wewe binafsi kwa kukubali kuwa mgeni rasmi katika uzinduzi rasmi wa Wakala hizi za Serikali ikiwemo Wakala ya Serikali Mtandao (eGA). Vile vile nichukie nafasi hii na kwa niaba ya watumishi wenzangu wa Wakala ya Serikali Mtandao, kukupongeza wewe Mheshimiwa Mgeni Rasmi kwa kuteuliwa kwako na Mh. Rais kuwa Katibu Mkuu Kiongozi.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Si nia yangu kurudia yale yaliyokwisha kusemwa kwenye hotuba ya Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, lakini itoshe tu kusema kuwa ujio wa Wakala ya Serikali Mtandao umelenga kutatua changamoto kadhaa ndani ya

Utumishi wa Umma. Katika kipindi cha miaka mitano, Wakala imejipanga kimkakati, kwa kushirikiana na Wizara, Idara, Wakala za Serikali, Serikali za Mitaa na wadau wengine, katika kutafuta na kutoa ufumbuzi wa kukabiliana na changamoto mbali mbali zilizopo katika utekelezaji wa dhana halisi ya Serikali Mtandao. Kama mjuavyo, Serikali Mtandao ni matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika kuboresha utoaji wa huduma kwa umma, kuhamasisha ushirikishwaji wa raia katika utoaji wa maamuzi yanayowahusu na kuwezesha uwepo wa Serikali iliyo wazi, inayowajibika na makini katika kutelekeleza majukumu yake kwa taifa.

Mheshimiwa Katibu Mkuu Kiongozi, Makatibu Wakuu, Watendaji wa Wakala na Wageni Waalikwa;

Licha ya uchanga wa Wakala ambayo kwa sasa ina watumishi wasiozidi watano, kuna mambo kadhaa yameshafanyika kwa ajili ya kujijenga kama taasisi katika kujiandaa kutekeleza majukumu yetu kwa mujibu wa mamlaka na miongozo iliyopewa Wakala. Baadhi ya mambo tuliyoweza kuyafanya tangu kuanza kazi tarehe 1/04/2012 ni pamoja na kuandaa Mpango Mkakati wa Miaka Mitano (2012/13 hadi 206/17); Kuanza kazi ya kukamilisha Tovuti ya Serikali Mtandao(e-Government Portal); kukamilisha Wavuti ya Wakala (www.ega.go.tz); kupata Ofisi za Wakala; Kuandaa Miongozo mbalimbali; pamoja na kuanza mchakato wa kufanya utafiti wa hali TEHAMA Serikalini (e-Government Baseline Survey). Napenda nichukue fursa hii kuwashukuru kwa dhati kabisa Mh. Waziri wa Nchi –OR-MUU, Katibu MkuuOR-MUU, Naibu Katibu Mkuu OR-MUU, Wakurugenzi pamoja na watumishi wengine wote OR-MUU kwa namna wanavyotusaidia katika utendaji wetu wa kila siku.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi

Katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku, Wakala ya Serikali Mtandao itatoa msukumo katika maeneo makubwa manne ambayo ndio yatasaidia kufikia malengo ya kuanzishwa kwa Wakala. Mosi, kupunguza gharama kwa kuhakikisha vifaa, miundombinu, mifumo yaTEHAMA Serikalini inashabihiana na gharama pamoja na ubora na tija ya huduma zilizokusudiwa kutolewa. Hili litawezekana tu kwa kuwa na mifumo ya pamoja ya TEHAMA pamoja na uwepo wa usimamizi thabiti wa miongozo na kanuni zinazosimamia matumizi ya TEHAMA Serikalini. Pili, kuhakikisha uwepo

wa matumizi salama ya TEHAMA bila kuathiri usiri na usalama wa taarifa muhimu za Serikali. Tatu, kuhakikisha kuwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali na Mamlaka za Serikali Mitaa zinaunganishwa na mtandao mmoja ili kurahisisha mawasiliano na matumizi sahihi ya rasilimali. Mwisho, kuainisha na kutoa kipaumbele kwa huduma ambazo zinaongeza uwazi na uwajibikaji na zile ambazo zinagusa maisha ya kila siku ya mwananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi

Pamoja na Wakala kujipanga vyema katika kutekeleza majukumu yake, silaha yetu kubwa itakuwa ni kushirikiana na Wizara, Idara za Serikali zinazojitegemea, Wakala, Serikali za Mitaa na wadau wengine katika utendaji wetu wa kila siku. Aidha, nitumie fursa hii pia kuwaomba Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu, Watendaji Wakuu wenzangu, Watendaji wote wa Serikali na wananchi kwa ujumla wao kutupatia ushirikiano na msaada wa hali na mali katika utendaji wetu wa kila siku.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, ***Makatibu Wakuu, Watendaji wa Wakala na Wageni Waalikwa;***

Naomba nisiwe msemaji ikizingatiwa kwamba nilipewa dakika tano tu, nichukue fursa hii kuwashukuru watumishi wa Ofisi ya Rais,Menejimenti ya Utumishi wa Umma, watumishi wa Wakala ya Serikali Mtandao kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku. Aidha, nitumie fursa hii kuzishukuru taasisi zote za Serikali pamoja na watendaji wao kwa misaada yao ya hali na mali wanayotupa. Kipekee, niwashukuru waandaji waliowezesha kufanyika kwa tukio hili pamoja na ndugu zangu wanahabari mliofika hapa.

Mwisho kabisa, nichukue fursa hii tena kukushukuru kwa dhati kwa kutenga muda wako kuja kujumuika na sisi katika tukio hili adhimu la uzinduzi wa Wakala za Serikali.

Ahsanteni kwa Kunisikiliza